**KISWAHILI**

**Tarehe: 19/Juni/2025**

**Wakati: 14h00’-16h00’**

NESA NATIONAL EXAMINATION AND SCHOOL INSPECTION AUTHORITY

# MWONGOZO WA KUKOSOA MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

**KIWANGO:** **Kidato cha Pili**

**MUDA:** **Masaa mawili (2)**

**ALAMA:** **...... /20** **CAMIS:** **...... /20**

**MAELEKEZO**

- **Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.**
- **Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu tatu:**
    - **Ufahamu (alama 5),**
    - **Sarufi na matumizi ya lugha (alama10),**
    - **Utungaji (alama 5).**
- **Mtihani huu unaundwa na maswali 10.**
- **Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.**
- **Tumia kalamu ya bluu au kalamu nyeusi.**
- **Kuhusu maswali ya kuchagua, weka mduara (0) kwenye herufi ya jibu lililo bora.**

**SEHEMU YA I: UFAHAMU (ALAMA 5)**

**Soma kifungu cha habari kilicho hapa chini kisha ujibu maswali yanayofuata:**

“Tuharakishe. Ujenzi wa choo umeanza,” Ikirezi aliniambia. Alikuwa akihema. “Mimi ni mgonjwa. Ningali ninaumwa na tumbo lakini nitajikaza,” nilimjibu. Hatimaye tuliwasili penye mkutano. Watu walikuwa wamejigawa katika vikundi tayari kwa kazi mbalimbali. “Tazama. Kila mtu ameanza kujenga choo isipokuwa sisi,” nilimwambia Ikirezi. Kiongozi wa kijiji alinisikia. “Msiwe na shaka. Nyinyi mtaokota taka zote zilizopo pale uwanjani. Baada ya hapo, mtafagia kando ya barabara. Kazi hiyo si ngumu,” kiongozi wa kijiji alisema. Mimi na Abatoni tulitafuta fagio. Tuliongezewa vijana watatu ili watusaidie kufanya kazi hiyo. Tulifurahia sana kushirikiana na wanakijiji.

**Maswali ya ufahamu**

**Kuhusu maswali ya kuchagua, zungusha mduara (0) kwenye herufi ya jibu lililo bora.**

1) Kichwa cha kifungu cha habari hiki kinaweza kuwa: **(alama1)**
    a) Ushirikiano katika michezo
    **b) Ushirikiano katika ujenzi wa choo**
    c) Ushirikiano katika ujenzi wa shule
    d) Ushirikiano katika uongozi
2) Ni kwa sababu gani Ikirezi alimwambia mwenzake kuwa na haraka? **(alama1)**
    a) Kwa sababu watu wengine walichelewa kufika
    b) Kwa sababu watu wote walikuwa wamechelewa katika mkutano.
    **c) Kwa sababu watu wengine walikuwa wameanza kujenga choo**
    d) Kwa sababu watu wengine walikuwa wamekosekana.
3) Mkuu wa Kijiji aliwataka Ikireze na mwenzake wafanye nini? **(alama1)**
    **a) Waokote taka zote zilizo uwanjani.**

b) Wasiende katika mkutano

c) Wasifanye kitu chochote

d) Wabomoe choo kilichojengwa.

4) Jinsi gani Ikirezi na wenzake walijisikia baada ya kushirikiana na wanakijiji?

**(alama1)**

a) Walikuwa na huzuni

b) Walishangaa sana

c) Walikuwa na huruma sana

**d) Walikuwa na furaha sana**

5) Toa muhtasari wa kifungu cha habari hapo juu katika mistari mitano.

**(alama1)**

**Mfano wa muhtasari:**

**Ikirezi na wenzake wakukwenda kusaidia wanakijiji katika ujenzi wa choo. Walijikuta wamechelewa. Walipofika mahali panapojengwa choo, mkuu wa Kijiji aliwapa kazi ya kuokota taka na kufagia barabarani. Walifurahi sana kwa kushirikiana na wengine.**

**SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (alama 10)**

6) Taja kinyume cha vielezi vilevyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo:

**(alama 2)**

a) Yeye anacheza <u>vizuri.</u> **Vibaya**
b) Kobe anaondoka <u>haraka</u>. **Pole**

**7)** Eleza kazi ya golikipa katika mchezo wa kandanda. **(alama 2)**

**Kazi ya golikipa kulinda zamu na kuudaka mpira ili goli lisiingie**

8) Tia tungo ifuatayo katika hali ya umoja . **(alama 2)**

- Vitabu vyangu ni vizuri

- **Kitabu change ni kizuri**

9) Tia sentensi ifuatayo katika wakati ujao, hali Kanushi: **(alama 4)**

- Wachezaji wote wanashiriki katika mazoezi

- **Wachezaji wote hawatashiriki katika mazoezi.**

**SEHEMU YA III: UTUNGAJI (alama 5)**

**10)** Andika barua kwa mwanafunzi rafiki yako MAHORO Ange anayesomea katika shule Jirani inayoitwa GS IKIREZI. **(alama 5)**

**Kwa kusahihisha ni lazima kuzingatia kanuni za kuandika barua ya kirafiki. (alama 5)**

- **Anwani ya mwandishi iliyo juu upande wa kushoto. (alama 0.5)**
- **Tarehe, chini kidogo ya anwani ya mwandishi (alama 0.5)**
- **Kutaja mwandikiwa, chini kidogo ya tarehe. (alama 0.5)**
- **Utangulizi/Salamu. (alama 1)**
- **Mwili wa barua/ Ujumbe kamili. (alama 1)**
- **Hitimisho. (alama 1)**
- **Saini/ sahihi na jina la mwandishi (alama 0.5)**

**Mwisho.**